



COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD

Tuesday, 17th June, 2025

Third Assembly – Fourth Session
THIRTIETH SITTING

[The County Assembly met at 11:00a.m at the County Assembly Buildings]
[The Speaker (Honourable Aharub Ebrahim Khatri) in the Chair]

PRAYERS

The Speaker (Hon. Khatri): Honourable Members, you may be seated. Yes, Clerk next Order Please.

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

STUDY VISIT BY STUDENTS FROM MTOPANGA SECONDARY SCHOOL

Good Morning Honourable Members. It is my great pleasure to warmly welcome the students and teachers of Mtopanga Secondary School to the County Assembly of Mombasa. We are truly honoured to host you here today. Your presence in this House signifies a keen interest in leadership, governance, and civic responsibility values that are crucial for building a stronger society and shaping a better future. As young leaders and future decision makers, I encourage you to remain curious, stay informed and continue asking the important questions. The Assembly you are visiting today is where elected leaders represent the voices of the people of Mombasa; I hope your visit will be both educational and inspiring. To the teachers accompanying them, we appreciate your guidance and dedication in mentoring the next generation. Once again, welcome to our County Assembly; may this visit leave a lasting impression and deepen your understanding for public service and democratic process.

[Applause]

Thank you very much. Honourable Members, today we have 57 students from Mtopanga.

1. Zahara Hamisi
2. Saumu Beja
3. Blessings Awinja
4. Ummi Umazi
5. Fatma Hassan
6. Hanifa Abdalla
7. Brenda Achieng

8. Zeal Nekesa
9. Bado Salma
10. Deborah Kai
11. Janipher Manga
12. Latifa Said
13. Sharon Mueni
14. Halima Sidi
15. Esther Pendo
16. Ushindi Kadzo
17. Zainab Yusuf
18. Ann Egesa
19. Erick Kitonga
20. Bonface Muema
21. Junior Mutembei
22. Bernard Changawa
23. Said Khamis
24. Dickson Kamanthi
25. Patrick Wangoni
26. Abel Tsuma
27. David Etale
28. Richard Boke
29. Mark Marwa
30. Kassim Shaban
31. Philip Ouma
32. Samuel Kombo
33. Erick Mwagandi
34. Nasir Masudi
35. Joshua Nyimbi
36. Antony Masha
37. Moses Said
38. Omar Edward
39. Fathiya Khamis
40. Halima Sidi
41. Mtenzi Kidongo
42. Hassan Mwamtunza
43. Ατημαν Mohammed
44. Jamil Macharia
45. Joel Rungua
46. Nicholas Tungwa
47. Dinice Mwaganda
48. Shima Mbetsa
49. Mitchell Sifa
50. Najma Ali
51. Munira Ndago
52. Shenga Bashir
53. Stephen Κατανα
54. Juma Amani
55. James Mutua

56. Florence Boke
57. Fiona Musyoki

Teachers:

1. Eunice Mwende
2. Geneveive Wekesa

Thank you very much and as I said earlier, 'Karibuni sana' Mombasa County Assembly.

[Applause]

Yes, Clerk next order please.

MOTION

ANNUAL SUB-COUNTY MULTI-SECTORAL PUBLIC ENGAGEMENT FORUMS

Yes, Honourable Jactone Madialo, MCA Mikindani Ward, please move the Motion.

Hon. Madialo: Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker Sir, I beg to move the following Motion;

AWARE THAT Article 174 of the Constitution of Kenya, 2010 outlines the objects of devolution, including to promote democratic and accountable exercise of power, foster national unity by recognizing diversity, and to give powers of self-governance to the people and enhance their participation in the exercise of the powers of the State and in making decision affecting them;

FURTHER AWARE THAT Article 10 (2) (a) of the Constitution emphasizes the national values and principles of governance including public participation and inclusiveness;

COGNIZANT THAT effective service delivery requires regular interaction between citizens, their elected leaders, and departmental officers for transparency, accountability, and citizen driven development;

NOTING THAT such forums shall provide an opportunity for departmental officers to respond to questions raised by the public regarding their mandates and service delivery, with the objective of strengthening transparency, citizen oversight, and participatory governance in line with the spirit and objects of devolution;

CONCERNED THAT there remains a gap in regular, structured engagement between county departments, elected leaders, and the public at the grassroots level;

I, urge this Assembly to RESOLVE that:

- a. The County Executive establishes an annual multi-Sectoral public engagement forum in each sub-County.*
- b. The forums shall be conducted once every financial year in each sub-County and be coordinated in a structured, inclusive, and transparent manner.*

c. The County Secretary develops and issues clear guidelines on how these forums will be conducted, beginning with the 2025-2026 financial year.

d. A comprehensive status report on the issues pertaining to mandate of the County Government shall be discussed and resolutions made during these forums shall be tabled in the County Assembly for adoption and implementation by the Executive.

Thank you, Sir.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Honourable Madialo. Second please?

Hon. Madialo: Honourable Priscillah Mumba will second.

Hon. Mumba: Thank you, Mr. Speaker. I stand to second.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Members. Honourable Members I now propose the question that the Motion by Honourable Jacktone Madialo on Annual Sub-County Multi-Sectoral Public Engagement Forums be considered by this Honourable House in the same terms as moved?

[Question proposed and agreed to]

And yes, Honourable Jacktone Madialo, please make your contribution to the Motion.

Hon. Madialo: Ahsante sana Mheshimiwa Spika pamoja na Waheshimiwa kwa kunipatia fursa hii ile sababu yangu kuleta Mswada huu hapa Bungeni inaweza kuwa na sababu nyingi lakini nitataja mbili tuu. Jambo la kwanza tukiwa makini na tukiangalia kila mwaka huwa tunapeleka bajeti kwa wananchi na pia tunapeleka yale makadirio ya maendeleo kwa wananchi ambapo inaitwa ‘ADP’ na tunapeleka kwa wananchi pia wanaweka wanasema mtazamo wao na baada ya hapo tukiangalia kwa makini huwa kuna jambo lengine huwa linatendeka na wananchi wanawekwa kando mpaka tena mwaka ukiisha tena tukianza tena mwaka mwingine tena tunakimbilia wananchi kuwaambia kwamba tuna bajeti ingine na ADP ingine. Kwa hivyo hawajakua na fursa ya kujiuliza ya kwamba kwa mfano mwaka uliopita sasa wananchi wale kujiuliza kwamba mwaka uliopita muliweka a, b, c, d kwa bajeti lakini je hiyo a, b, c, d wamefanya gani?

Kwa hivyo Mswada huu unapeana fursa ya kwamba katikati ya mwaka baada ya sisi kuendea wananchi na ADP na pia na bajeti na kuwaambia kwamba watafanya wa hili na hili na hili. Mswada huu unapatia fursa sasa wananchi ya kuuliza the utawala moja kwa moja mashinani ya kwamba tuliambiwa kwamba tutajengewa barabara pale, tutajengewa daraja pale, tutajengewa ECDE pale, mazingira idara itafanya hivi pale je imefikia wapi ama mbona hamjafanya? Sasa wakati huo wale katika idara maana Mswada huu unataka kwamba idara zote ambapo ni kumi pamoja na Waheshimiwa wa Wadi kutoka eneo Bunge fulani pamoja na wananchi wao wakue pamoja kwa kikao. Sasa Waheshimiwa MCAs wakati huo ndiyo watakuwa kama kwa kingereza na hiyo *umpires* ama *referee* ya kupeana na nafasi kwa wananchi kuuliza maswali na maswali hao yajibiwe moja kwa moja na wale kutoka kwa idara. Ya pili, kwa nini nimeleta Mswada huu? Mheshimiwa Spika ninaomba uni...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Order Honourable Mwamwiri Majority! Leader! Please! Order!

Hon. Madialo: Ahsante Mheshimiwa Spika. Jambo la pili, kwa nini nimeleta Mswada huu; mara nyingi sisi Waheshimiwa tunabeba mizigo ambapo si yetu na tunapokea lawama nyingi sana mitaani. Kwa hivyo hivi vikao vitatusaidia na vitaelimisha wananchi wajue ya kwamba kazi yetu ni gani? Na kazi ya wale utawala ni gani? Kwa mfano mara nyingi kama kuna barabara ambapo imeharibika wanafikiria kwamba ni sisi ndio tuna pesa ambapo yatakikana kujenga, kama hakuna mataa ukweli wa mambo ni kwamba kila Mheshimiwa hapa ambae amechaguliwa kwa Wadi ataniambia kwamba meneja wa Wadi wao amekaa mahali akiwa ametulia na roho yake iko safi maana anajua kwamba shida anayepokea ni nani, ni Mheshimiwa. Kwa hivyo.... samahani *Ward Administrator*, ahsante kwa kunirekebisha, *Ward Administrator* wanakaa pale wakijua kama saa hii kuna mataa yameharibika pale mtaani hawaendei *Ward Administrator* wanatujia sisi.

Kwa hivyo hili jambo hili tunapoelekea wakati wa uchaguzi lazima tuwe werevu, lazima tuwe wajanja mahali ambapo si kwetu wananchi tunawaambia kwamba hio si yetu lakini mahali ambapo ni yetu tutapata *credit* pia wewe unajua vile ambavyo utacheza huo mchezo. Kwa hivyo jambo hili litatusaidia ili wananchi wahudumiwe katika njia ya ukaribu na pia ni kulingana na sheria na katiba ambapo inatuelezea kwamba lazima wananchi waende wakatumiwe mpaka kule nyanjani. Ahsante sana Mheshimiwa Spika na naomba kwa unyenyekevu na Waheshimiwa mkapate kuunga mkono Mswada huu kwa sababu moja kwa moja Mswada huu utasaidia na pia itasaidia kazi na pia *executive* wakigundua ya kwamba wakiweka bajeti na wataenda kuulizwa moja kwa moja na wananchi kule nyanjani watafanya kazi lakini wakijua ni sisi tu tutakuwa tunakuja hapa tukiulizwa maswali tukipeana sijui *Committee of Implementation* na hakuna kitu inakua *implemented* na saa hii tukiwatega na wananchi watachangamka. Ahsanteni.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Jactone Madialo. Yes, Honourable Priscillah Mumba please.

The Chief Whip (Hon. Mumba): Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii. Kwanza kabla sijachangia ninataka kushukuru watoto wa Mtopanga ambao wamekuja kututembelea katika Jumba hili. Tunashukuru kuwaona mkiwa na walimu wenu na upendo wa kutaka kujua yanayoendelea katika Bunge la Kaunti na viongozi wake; mujisikie huru muweze kupata mafunzo ya kuja kuwajenga na kuweza kuwa viongozi kama tulivyo hapa maana hata sisi wakati mmoja tulikuwa watoto kama nyinyi na tuliweza kusoma na tuliweza kuweka familia zetu juu na tukaweza kuwa watu wa aina unavyotuona leo. Kwa hivyo karibuni sana na mujisikie huru; nikitaka kuchangia jambo hili ambalo Mheshimiwa Madialo amelileta hapa Bunge ni swala muhimu sana na Mheshimiwa Spika ni wakati mwafaka tutakapo kuwa tunapitisha Mswada kama huu tuweze kuhakikisha utekelezaji umefanyika. Kwa sababu shida kubwa ya Jumba hili ni kuwa tunapitisha Mswada mizuri sana lakini wakati wa kuifuatizia kuwa ifanyike hapo ndio kuna kuwa na udororeshaji.

Swala hili ambalo limeletwa na Mheshimiwa Madialo kusema kweli katika sisi viongozi wa Kaunti ambaye ni ma MCA's ninaweza kusema hili ndilo donda sugu linalo tutandika katika mitaani ambapo watu hawaelewi majukumu yetu. Na tutakapo kubali mambo kama haya yafanyike tutakuwa ni njia moja ya kujirahisishia kazi zetu na kupunguza lawama katika Wadi zetu. Kwa sababu kuna majukumu ambayo hata sio yetu sisi lakini sisi ndio tunabandikwa na kulaumiwa; wakati sisi tunapitisha mambo hapa ni wajibu tuhakikishe yale mambo yamefanyika kule nyanjani kwa kufuatizia. Yafuatiliwe Kamati ya Utekelezaji iweze kukaza mkono kwa sababu hakika jambo hili likitimia kulingana na vile ambavyo Mheshimiwa Madialo amelileta hili litakua limeturahisishia kazi kubwa sana wakati tunakuja kipindi cha siasa.

Mheshimiwa ambaye ni MCA ndiye anaye laumiwa katika majukumu yote ya Wadi na kustajibisha wakati tunapo kuwa katika mikutano ya nyanjani huwa sisi hatutajwi kuwa tumepitisha katika Bunge Mswada gani, tumepitisha pesa gani, tunafanya kazi gani? Kwa sababu yale yote yanayofanyika kule nje nyanjani ninavyojua yanatokana na hili Bunge, maana tukiwa sisi hatukupitisha fedha yoyote ndani ya hili Bunge katika Mswada wa bajeti alafu kwa mwaka mzima hakuna jambo litafanyika la maana. Lakini kwa sababu tukishapitisha hapa huwa tukiwa nyanjani hakuna anaye tutambua kuona kuwa hawa walipitisha suala hili. Kwa hivyo wakati kutakapokuwa kuna mikutano kama hii itajaribu kueleza tulipitisha jambo hili na wananchi waliona jambo hili, Je jambo hili limefanyika ama bado? Kwa hivyo hili si jukumu tena na MCA ni jukumu la *Executive* kujieleza kuwa kitengo hichi cha hii pesa ilitengwa mbona hii kazi ya hii kufanyika. Moja kwa moja pale utakuwa katika hali ya kuwa umejiondolea lawama kwa wale ambao watakao kuwa wako katika ule mkutano. Maana wengi huwawakiona majukumu hayajafanyika katika Wadi lawama huwani MCA.

Lakini mambo yakiwa yamefanyika katika Wadi hakuna jina la MCA hiyo ni ukweli mtupu! Hakuna jina la MCA linalotajika katika majukumu ya Wadi ambayo yanafanyika na hali kazi zetu ni sisi hapa katika Bunge ni sisi ndio tunabeba uti wa mgongo wa bajeti ambayo tunayoipitisha. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika mimi nimeunga mkono na imekuja kwa wakati ambao ni mwafaka kwa sababu hata saa hii tuna kilio cha kutaka vikundi vya vijana na kina mama waweze kupewa pesa zinazotakikana kuendeleza majukumu yao katika Wadi na pesa hizi ikiwa sisi wenyewe hata tukapitisha na tukose kuwa na Mswada kama huu jambo kama hili halitafanyika tutapitisha senti na yale tunayataka yafanyike hayatafanyika nawaambia. Ikiwa hatutaweza kuwa na mabaraza kama haya ya kuweza kusisitiza *Executive* ieleze kila thuluthi iliotamka katika mwaka wa makadirio je wametimiza majukumu?

Katika Wadi yako umehakikisha kuwa madawa yako yaliletwa kwa sawa? Umehakikisha kuwa barabara zako zilitengenezwa kwa wakati mwafaka? Uhakikishe kuwa unaileza watu wako barabara yangu fulani ilikuwako katika bajeti ndiposa mimi nikahusika katika kutengeneza bajeti. Lakini mwaka umeishana barabara sikuiona. Wananchi wakiwa pale watajua kumbe kosa ilikuwa si lako kosa ni la wale *executive*. Lakini wakati tutakapo kuwa tunanyamaza kimya turudi bajeti hadi bajeti then tutakuwa sisi tunajifunga kitanzi wenyewe. Kwa sababu mwananchi atakuuliza kama kweli kulikuwa kuna tatizo mbona hukuwai kufanya baraza ukaja ukatueleza ndiposa na sisi tuwezakueka sauti. Kwa hivyo Mheshimiwa Madialo ninakupongeza sana na Mwenyezi Mungu azidi kukupa hekima na jambo hili ulitotufanyia limekuja kwa wakati mwafaka tumebakia kipindi cha mwaka moja na nusu na tusipoonekana kuwa kama tumefuatilizia yale majukumu yetu katika Wadi zetu then nawaambia nikiwa mmoja ambaye ni mkongwe wa Jumba hili niko hapa mara tatu. Kwa hivyo ninaelewa yale makombora unayo kwenda kukutana nayo katika Wadi ambayo hutayatarajia na yatakua katika Mswada huu yatatukingia yale makombora. Mheshimiwa Spika ahsante sana.

The Speaker (Hon. Khatri): Ahsante Mheshimiwa Prischillah Mumba. Yes, Honourable Morgan Matsaki from Mtopanga Ward? Yes, Honourable Jactone Madialo?

Hon. Madialo: Ahsante. Ninaomba msamaha sana ya kwamba sikutambua shule na wageni ambao wako hapa, karibuni sana na kwa sababu Mheshimiwa wenu ni rafiki yangu sana na hua anatetea sana maslahi ya Wadi mahali munatoka; kwa hivyo naomba radhi kwa sababu nilipitiliwa ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Honourable Jactone Madialo? Yes, Honourable Morgan Matsaki from Mtopanga Ward.

The Leader of the Minority Party (Hon. Matsaki): Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwanza kwa kunipa nafasi hii. Pili, wacha nikushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kukaribisha vijana kutoka eneo langu la Mtopanga Mungu akubariki sana. Karibuni sana hili ni Jumba la mazungumzo ambayo Miswada kama hii munayoisikia na nyinyi muko shule, sisi pia tulikuwa hapo na nina matumaini hapo mulipo munamaliza kuna wakurugenzi, kuna wale ambao watakuja kuchukua nafasi hizi zetu ambazo tuko nazo tunapozeeka. Kwa hivyo mujisikie huru na muko na maswali ya kuuliza mna haki ya kuuliza wafanyi kazi wako hapa kwa kuulizwa maswali. Mheshimiwa Spika nikisimama ninasimama kuunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa mwenza Mheshimiwa Jactone Madialo, ni hoja nzuri sana na laiti ingekua ni vyema wakati tulipoingia Jumba hili ingekuwa ilikuwa ni hoja ya kwanza kuingia Bunge hili. Kwa sababu ki ukweli sisi Waheshimiwa mashinani kama vile Mheshimiwa mwenza Mheshimiwa Prischillah Mumba na Mheshimiwa Jactone Madialo kwa kweli tunapata shida sana mashinani kwa sababu wananchi zaidi ya yote hawajui majukumu yetu. Sisi majukumu yetu zaidi ni kwa ufupi mikutano ya kiserikali ama ya ki Kaunti, ni lazima sisi tuhusishwe na tuweze kuifanya na mambo mengine mengine.

Mkutano huu kwanza nikiutilia mkazo zaidi ufanyike, hii hoja la kwanza ni vyema sana *Executive* waweke huu mkutano ili waeleze bajeti iliyopita ile miradi ambayo walikuwa wameiweka katika kila Wadi; ijapokuwa itakuwa kwa *Sub County* lakini itakua ni ulazima sana kila Mwakilishi Wadi aweze kupata fursa ya kuambia wananchi wote wa Wadi ile waweze kuhudhuria mkutano ili lile jambo ambalo kuwa limepangwa ama ule mradi waelezewe ulifanyika au la na haukufanyika ni kwa sababu gani? Kwa sababu bajeti twaipitisha sisi hapa lakini mengi ni wananchi wajue haswa kinachofanyika mashinani. La pili, itakuwa ni rahisi kwetu sisi kabla hatujaingia nyanjani na zile ADP ama bajeti zetu za kuwasomea wananchi itakua imetupatia nguvu kwetu sisi tunapofika pale kwa ile mikutano yetu tunayofanya; wao itakua ni rahisi sana kwamba kweli mkutano ulikuwako wa *Executive* na walituelezea bajeti na hii bajeti inayokuja ni jambo gani wanauia kulifanya. Kwa hivyo mimi Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono jambo hili na itakuwa ni bora zaidi Bunge hili kwa Waheshimiwa wenza pia wazidi kuunga mkono kama vile sisi tulivyosimama Waheshimiwa wenzao wauunge mkono na hili jambo lichukuliwe hatua mwafaka kwa sababu twapitisha kweli Miswada mingi na mizuri lakini utekelezaji ni shida kama Mheshimiwa mwenza alivyozungumza. Kwa hivyo nimesimama kuunga mkono na nashukuru sana Mheshimiwa Spika kwa nafasi hii umenipatia. Karibuni sana wana Mtopanga, ahsante sana. Karibuni sana wanamtopanga.

The Speaker (Hon. Khatri): Ahsante sana Mheshimiwa Morgan Matsaki. Yes, Honourable Milka Moraa Ngare?

Hon. Ngare: Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity. Before I debate on the Motion, I would like to also welcome the students from Mtopanga Secondary School where Honourable Morgan Mastaki represents and also to say that you have always given enabling environment Mr. Speaker where we have regular visitors of children coming from all over Mombasa County. I know the teachers and students by the time they are leaving here; they will know that we have an Honourable Speaker and a half! They will go back smiling, so teachers thank you for exposing the children to practical or life experience, and as a former teacher I know we used to call this subject, social studies I do not know whether that is the thing because now we have Curriculum Based Competence but whatever it is welcome and feel at home. Mr. Speaker, I rise to support the Motion brought to this House by Honourable Jactone Madialo of Mkindani Ward and I think it is a very important Motion for us and for the citizens of Mombasa one other than questioning on the budget issues and other things.

We know that this will be creating transparency and accountability from both sides...

[Interruption]

Hon. Ngare: Thank you, Honourable Patrick Mbelle. Public forums will hold leaders accountable and citizens can question on things that are happening within the County. For example, they can question on why we have water coming only twice a week or not coming at all? Why do we have flooding in this area? What is happening? For example, health officers from the Sub-County level can be able to respond to issues like why do we have *Chikungunya* right now? What is the County government doing to prevent this very disabling disease? Why is this not happening? Why do we not have officials doing flogging, do we call it flogging, for the County of Mombasa so that the citizens do not have such kind of issues. Then we know that Mombasa as a County, to tackle complex issues like what Honourable Prischillah Mumba talked about of lack of youth employment, revolving fund issues which have become a thorn in the flesh. Why do we have these things lacking? Why, for example, do we have lack of child care centres and other Counties have already had them in place, yet in this very House we passed a motion on creation of child care centres for women in the market. Why is it taking so long? So, citizens can challenge and ask questions on the same and they will be able to give answers other than other issues also that have come up from my fellow Members. So, this will enhance collaboration between community leaders and County officials to improve service delivery. It is an important Motion that we should take seriously and that should be implemented by the County Government after we have passed from here. So generally, collaboration will be a good thing between the multi-sectoral departments. Thank you, Mr. Speaker.

[Applause]

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much, Honourable Milka Ngare. Yes, Honourable Athman Mwamwiri, the Leader of Majority Party. Please make your contributions.

The Leader of the Majority Party (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika awali ya yote nitambue na kukaribisha wanafunzi wa Mtopanga ambao wapo kwa ziara ya ki elimu kujifunza mali ya utawala na utenda kazi hususan wa Bunge na Wabunge wake katika Bunge la Mombasa. Niwakumbushe pia ya kwamba Mwakilishi wenu, Mheshimiwa Morgan Mastaki ambaye ni Kiongozi wa Walio Wachache katika Bunge hili na amekuwa siku zote akisimama kwa ajili ya mapenzi na maendeleo ya watu wa Mtopanga; kwa hivyo salamu hizi zimregeshe majumbani hususan kwa wazazi wenu ya kwamba wanae mwakilishi ambae anasimama barabara kwa minajili ya watu wa Mtopanga...

[Applause]

Mheshimiwa Spika, hoja hii ni hoja adimu sana ambayo kwetu sisi kama Bunge inatuheshimisha, kwa hivyo nimesimama kuunga mkono hoja hii. Kabla kuchangia Mheshimiwa Spika kuna Mheshimiwa hapa alikua na dukuduku na utangulizi wa Mheshimiwa Jactone Madialo hususan katika matumizi ya lugha ya Kiswahili na akamtilia shaka alipotaja konsonati zile ya kwamba huenda amezikanganya. Lakini nimwambie tu Mheshimiwa ya kwamba kile ambacho Mheshimiwa amekosea kidogo katika kutaja konsonati ya tatu ambayo amesema 'ka' katika Kiswahili ile tunaiyongeza na 'h' na tunaitamka kama 'cha'. Kwa hivyo hatusemi 'ku' kama wanavyotamka Waingereza *a, b, c* sisi tunasema '*a, bu, cu, du*' ahsante Mheshimiwa Spika nadhani hilo limerekebishika. Mheshimiwa Spika mamlaka ya serikali ya Ugatuzi unaposoma sheria zake sehemu ya 44 inatafsiri vizuri majukumu ya katibu wa Kaunti lakini zaidi ya hayo pendekezo hili liko katika mgongo.

Zaidi tunaposoma sehemu ya 51 ya County Government Act ambayo majukumu haya yako chini ya utawala wa gaturu dogo chini ya kiongozi ambaye tunamfahamu sote kama Sub County Administrator na Ward Administrator wake na Village Administrator. Hawa wanapaswa ya kwamba wawe wakisimamia na kuendesha mabaraza haya kupeana taarifa kwa wananchi yale yanayojiri katika serikali yetu ya kimaendeleo, ya kielimu, ya kimikopo, ya kibajeti na kadhalika na vile vile kuchukua kwa hayo kutoka kwa wananchi katika zoezi hili. Vile vile sisi kama Waheshimiwa na wawakilishi wa sehemu zile hatuwezi kukimbia moja wapo ya jukumu letu la kwamba sisi ni wawakilishi na katika uakilishi Mheshimiwa Spika taa zinapogoma kuwaka lazima tutafwatwa tupewe taarifa ile. Si jukumu letu kufanya baraza kujadili kuhusu taa, lakini ni jukumu letu kulifikisha hapa na kuuliza chini ya mwongozo wa Kamati husika kwa nini taa katika sehemu ile haiwaki na jawabu tutakalopewa lazima tuliregeshe kule kama jukumu la uakilishi ambalo tumepewa kipao Kikatiba Mheshimiwa Spika.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika swala hili ambalo Mheshimiwa amelipendekeza liwe na mpangilio rasmi ya kwamba tunajua kila mwezi wa sita wa kila mwaka zoezi hili linafanywa katika ngazi fulani, mahali fulani ili wananchi waweze kujiandaa, kujitayarisha na kuja kuuliza yanayowasibu. Vile vile Mheshimiwa Spika itakuwa moyo tunapokuja katika maswala ya utengezaji bajeti na vikao vya bajeti na vikao vya bajeti watakuja wakiwa na ghera ya kwamba yale ambayo huchangia kuna mahali sahihi pa kufikishwa na kuna mahali sahihi hupata majibu yanavyostahiki. Hivyo kuja kuchangia ujenzi na maendeleo ya serikali yao wanakuwa na moyo kujitokeza tofauti na sasa Mheshimiwa Spika mahaba ya wananchi wetu yako chini katika kuchangia utendakazi wa serikali yetu kwa sababu hiki kipengele cha kuregesha majawabu kwao hakitendewi haki. Kwa hivyo nasimama kuunga mkono na nahimiza waheshimiwa wenza tuweze kuunga mkono hoja hii. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Ahsante Mheshimiwa Athman Mwamwiri. Yes, Honourable Abdulrahman Hussein from Mji wa Kale Ward?

Hon. Abdirahman Abdikadir: Thank you, Mr. Speaker for giving me an opportunity to contribute to this very important Motion that is before us today. Allow me to first and foremost extend my warm welcome to the students from Mtopanga Secondary School, *karibuni sana*. Mr. Speaker, I have noted with a lot of concern the unanimous support that this Motion has received from all the Members and my message perhaps to those who intend to go against it is that it is easier to argue against gravity than to argue against this Motion today. Mr. Speaker, Chapter 1 of the Constitution talks about Sovereignty and the Supremacy of the Constitution it says that Sovereign power belongs to the people and may be exercised directly or indirectly. Directly in the sense that the public themselves can take it upon themselves to demand for better governance and accountability, or it might be delegated to us as leaders of both the Assembly and the National Assembly as well.

Mr. Speaker, this particular Motion today underscores the importance of that tenet of our Constitution, it says it gives the public an opportunity to rather exercise their own powers of holding elected leaders of holding the executive accountable for the promises that they have made, either through the Annual Development Plan (ADP) or other public forums. It provides a forum of engagement; it provides an opportunity to take stock of what has been done and what has not been done. Mr. Speaker, sometimes i fail to give sufficient answer to my residents in Old Town when they ask me why they have not received water for the past two weeks?! When they ask me when this road is going to be done?! When they ask me why we have insufficient lighting in some areas?! Mr. Speaker, I do my best to bring their particular grievances to this particular House but sometimes those grievances are not addressed well by the executive.

Mr. Speaker, such forums will be an opportunity for us to allow the public to also understand our role as elected leaders; that forms the basics of civic education. Mr. Speaker, more often the public, normally they are, I will not say that they are hard on us but I will say that they are misinformed on the roles that we engage and normally we do not get an opportunity to tell them our roles are limited to legislation, to representation and oversight. Mr. Speaker, such forums will be a forum to tell them that indeed that particular road that is not working well in Kuze and is not as a result of my lack of commitment but it is a result of the executive not undertaking the development that they have promised. Mr. Speaker, our public participations have been reduced to empty talks and I have managed to attend nearly most of the public participations that we normally conduct during important budget processes. Mr. Speaker, the public do not have, they do not have faith that whatever they raise or issues that they raise in the public participations are considered. They normally take it for an empty talk Mr. Speaker and it is high time that this changes and with this particular Motion, it will for certain be a platform where the public is given an opportunity to also question that's why their grievances, why their interests that have been captured in the ADP, that have been captured in various public participation forums have not been undertaken. Mr. Speaker, lastly, this is a very critical piece of legislative agenda that I think should go beyond this House and i urge my colleague, Honourable Jactone Madialo, to also consider petitioning the Senate and having this particular Motion be enacted in the County Government Act. It should be a legislative piece that should be enjoyed across all our 47 Counties, Mr. Speaker. With those few remarks, allow me to support this Motion with every breath that I have. Thank you, Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much, Honourable Abdulrahman Hussein. Yes, Honourable Franklin Makanga from Chaani Ward.

Hon. Makanga: Thank you Mr. Speaker. From the onset, I rise to support the Motion and I also take this opportunity to welcome the students from Mtopanga Ward, a Ward that is represented by our elder, Honourable Morgan Matsaki who has consistently advocated for the welfare of Mtopanga residents. So again, congratulations Honourable Morgan Matsaki and we are praying that for you it is not one term, it is two terms...

[Applause]

Honourable Speaker, I rise to support this Motion that has been brought to this House by Honourable Bishop Jactone Oluoch Madialo who I believe has not only...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Jactone Madialo, are you on a point of information?

Hon. Madialo: A point of order.

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Yes.

Hon. Makanga: Honourable Speaker, maybe he can cite the Standing Order because he is the mover of this Motion and I am supporting his Motion so I do not know why again he is upstanding? Maybe he can tell which Standing order.

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Honourable Frankline Makanga. Yes, Honourable Jactone Madialo.

Hon. Madialo: I stand on Standing Order 143 to ask that why is Honourable Makanga always interested in Oluoch? What interest does he have in it?

Hon. Makanga: Honourable Speaker, I think that Standing Order needs to be read out. You know he is a man of God and he cannot mislead this House.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, you can continue Honourable Frankline Makanga?

Hon. Makanga: Thank you...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, continue Honourable Makanga.

Hon. Makanga: Thank you Honourable Speaker again for protecting me. As earlier said, I am grateful that the Bishop who happens to be my close friend having considered coming with this motion, I believe also he has been inspired because he is a man of inspirations and the Holy Spirit must have inspired him. I know Honourable Milka Ngare knows what that means. Honourable Speaker, I rise to support this Motion. In regards to the Article 174 of the Constitution of Kenya, 2010 which Honourable Speaker states the objects of devolution, we being a Country government, when we are performing our roles as a House we should be guided by what Article 174 states as regards the object of devolution. Honourable Speaker, it is outright that this Motion brings forth accountability on the part of the executive and bringing to an end the spirit of public relations, the spirit of public utterances that at the end of the day, they add no value to the lives of our people. Honourable Speaker, the essence of accountability in any leadership is meant to drive performance as we stand here today, we are three years into our leadership, into our first tenure because some of us are coming back for the second term and the third term, God willing but as it stands now three years down the line, we have very minimal record of what this government has performed to the people of Mombasa. Honourable Speaker, unless we have such forums, where the leadership led by the executive will take accountability of what they have done with the resources that have been allocated to them by this Honourable House. Honourable Speaker, accountability builds trust right now; residents of this County have lost trust in their leadership, have lost trust in their leadership in the sense that you go to forums, you will hear all sorts of words and not only in Mombasa. Honourable Speaker, the reason why right now we have *Kasongo* and one-time songs out there is because the residents of this country have lost trust in their leadership both at the County level and the national level.

[Interruption]

Honourable Speaker, please protect me from Honourable Abdirahman; he is one person who always, when he sees me standing, chooses to stand just to disrupt my speech.

The Speaker (Hon. Khatri): Take your seat, Honourable Makanga.

Hon. Abdirahman Abdikadir: Mr. Speaker, I think I'm entitled to stand. I did not disrupt him, but rather am standing on a point of information.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes.

Hon. Abdirahman Abdikadir: Mr. Speaker, I have a clip in my phone of a function that happened yesterday and I heard the right Honourable Makanga rather cheering and saying, ‘kumi bila break! Kumi bila break’ and right now I can hear him lamenting on the status of our County. Mr. Speaker, I do not know if it's lapses of memory, I do not know whether it is hypocrisy, I fail to understand what that is. He has been cheering at the forefront of a forum that happened yesterday but right now he is complaining that this particular government has done nothing of late. Mr. Speaker, I think he needs to come clean and substantiate those sentiments of his. Thank you, Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Honourable Abdirahman for that, but Honourable Abdirahman, I do not think you are allowed to Table that evidence here and as far as I'm concerned, I have not heard that, but the Honourable Member can testify that himself. Yes, Honourable.

Hon. Makanga: Honourable Speaker, I happen to be amongst the few wise men remaining under the sun and I choose not to divert my attention to address the Honourable Member who happens to be yesterday he was in hospital. I'm wondering where he is getting the energy; you are actually going against medical advice you are supposed to be at home resting. Honourable Speaker, as I proceed with my submission, I have said and again I say, when it comes to issues of leadership and accountability, this is not something that we can play games with and neither can we draw comics into it. Honourable Speaker, accountability must be made a priority in this leadership and in this government; even as I come to the close of my submissions, I want to urge Honourable Madialo that this Motion that he has brought in this House today is meant to restore the trust, the trust by the people of Mombasa, the trust by Kenyan citizens who are paying taxes so that they are able to see government. Honourable Speaker, the same accountability is meant also to help improving decision making right now, we are in a situation where decisions are curtailed. As much as we may choose to be open-minded, to be visionary, to come up with a program that are meant to improve the lives of our people, when those decisions are made here, when recommendations are made here and resolutions made by this House, they are not implemented because we have a poor decision-making system in the leadership that we have in this County.

Therefore, Mr. Speaker, a time has come that we bring these executive leaders and ourselves in those forums so that each one of us can tell what they have done for the period of three years to the people of their Wards and also the Executive, they have a position to say how much they have used even to serve the people and what has not been used and why it has not been used because we have so many issues with us in our communities that it's so shameful that times we go into meetings and all you are left with is an egg on your face because you do not have anything to tell the people. *Umebaki na propaganda na PR nyingi na kucheka cheka ovyo. Kwa hayo mengi Mheshimiwa Spika mimi naunga mkono hoja hii na ipitishwa na ifanyiwe kazi. Na nikirekebisha Mheshimiwa Madialo amesema kwamba tuiptishe hii kwa sababu tuko karibu ka kampeni, hii hatupitishi kwa sababu tuko karibu na kupigiwa kura. Hii tunapitisha kwa sababu ni haki ya wananchi wa Mombasa kupata viongozi wanaojielewa wenye hekima na mimi nikiwa mmoja wao. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.*

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you ahsante sana Mheshimiwa. *Yes, Honourable Allen Katana from Shanzu Ward.*

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika kwanza uniruhusu nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pili, niwakaribishe wasomi kwanza Spika nafikiri sitakasirisha mtu nikimkaribisha mwanangu

anayeitwa nani wa Katana namkaribisha huyo zaidi kushinda wote na nimpe motisha ama nimpe changamoto ya kwamba Katana pia inawezekana akawa Mheshimiwa. Kwa hivyo atakapo fanya bidii nafasi kama hizi kama vile Mheshimiwa wa Mtopanga alivyo sema tunazeeka na nafasi kama hizi zitawahitaji. Mheshimiwa Spika nimesimama kupinga swala hili lililoletwa leo na inanihuzunisha sana, nimesimama kwa huzuni kubwa sana ya kwamba mwananchi masikini aliyeamka tarehe ile sisi tuliyopigiwa kura akatupa kazi akiwa na imani na matumaini ya kwamba huyu kiongozi wetu tuliempa kura zetu nyingi, ataenda kutusimamia na kupigania haki zetu kumbe kiongozi yule atakuwa muoga wa majukumu yake mpaka ayarudishe tena. Mheshimiwa Spika, Katiba yetu kifungu cha 195, imetupa sisi kama madiwani nguvu sawiya na korti kuu la Kenya hii, tunauwezo wa kuwaita viongozi wowote wa tabaka lolote na kuja kuwauliza ni kwa nini hili na hili halikufanyika?

Mheshimiwa Spika nataka ileweke kwamba hawa executive tunaowataja hapa Mheshimiwa Spika, wao hutayarisha bajeti tena wakapitia huko nyanjani, wakatuletea sisi tukarudi tena kwa *validation* tena tukarudi tukapitisha vitu vile. Mheshimiwa Spika tunahaki ya kusema bajeti ya mwaka jana muliyo leta vitu vyote tulivyo pitisha hamukutengeneza na kwa hivyo hii bajeti yenu rudini nayo mpaka mutafute pesa miradi iliyokuwa ya mwaka jana muiteengeze. Sisi tuko hapa tunalipwa mishahara ya walipa ushuru, wamekalishwa kwa vikao, executive wanawakalisha sisi wenyewe pia tunaenda kuwakalisha na imefika wakati wa sisi wenyewe kusimama na kutowasingizia wananchi. Nimeona ombi lake la kwanza Mheshimiwa Spika ni uzungu mwingi wa kujirudia na hakuna ajenda muafaka hapa Mheshimiwa Spika. Kitu cha kwanza alichobadilisha lugha katika sentensi yake ya kwanza, ameandika *establish an annual multi sectorial* la pili ameandika *once a year*, mimi sijasoma sana *annual na once a year* kuna tofauti gani pale, imewekwa ati ni ajenda ya pili ndio zionekane ni ajenda mbili tofauti. Mheshimiwa Spika, tutakapo itisha vikao, wale *executive* wenyewe wanakuja na magari milioni sisi wenyewe tutachoma mafuta kwenda kwa mikutano ni pesa ya mwananchi masikini inatumika vibaya kwa mikitano mingi ambayo haifanyiki. Hii mikutano mingi ambayo *executive* wakiifanya, wanaifanya kwa Ward level nimehudhuria kadhaa, wananchi wenyewe hawaji kwa akili ya kwamba tulimuandika MCA mwenye akili atapigana na haki yetu. Mheshimiwa Spika nisiongee sana kwa sababu sisikii vizuri lakini...

[Applause]

Nimalize kwa kusema hivi Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Order! Order Honourable Madialo! Let the Honourable Member make his contributions please; you will have your chance to reply Honourable Madialo.

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika unilinde. Unajua Mheshimiwa Spika, mtu unayemwambia ukweli ni sawa na mwenye upele kujikuna hata ukimwambia asijikune, atajikuna tu. Sasa hivi Mheshimiwa Spika, tena leo tumebahatika nashukuru tuna wanafunzi na walimu ambao watatoka hapa kama mashahidi ya kwamba kazi waliyotupa hatuiwezi mpaka tunawarudishia. Ahsante Mheshimiwa, napinga tena kwa sauti kubwa. Ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes, Honourable Hamida Noor?

[Interruption]

Yes, are you on a point of information?

Hon. Makanga: Yes, Honourable Speaker.

The Speaker (Hon. Khatri): But the Honourable Member has already submitted his, you cannot talk two times in a Motion.

Hon. Makanga: Honourable Speaker, it is a point of information.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes.

Hon. Makanga: From a medical perspective Honourable Speaker, where I happened to have gone to school, I have practice for the last ten years. Honourable Speaker, anybody who confesses that he is sick it is very important that we consider expunging whatever he has said *kwa sababu inaweza kuwa kutosikia vizuri kwake ni shida ya akili Mheshimiwa Spika. Kwa hivyo yale ambayo amesema itakuwa bora kama Hansard itakuwa deleted kwa sababu aliyoyasema hatuna uhakika kama ako na capacity ya kuzungumza maneno hayo katika Bunge hili. Ahsante.*

[Applause]

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Makanga and I know you happened to be a doctor, but yes Honourable Katana you can substantiate that.

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika, siku nyengine kama Mwenyezi Mungu akitujaalia kurudi mtu akijiita daktari itisha makaratasi, madaktari wengine ni madaktari wa mitishamba na kanuni zetu za kudumu zina sema utakapo anza kujieleza kwa lugha fulani hakikisha unatumia lugha hiyo hiyo mpaka mwisho. Lakini Mheshimiwa Spika nakushangaa pia wewe kwa hekima yako unawacha anamaliza maneno ambayo ni ya hekima, nimeongea kwa ajili ya Nyumba hii anayachanganya kwa kuwa yeye ni daktari wa miti shamba. Ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): I think Honourable Katana you should just clarify, *kuwa wewe si mgonjwa wa kichwa*, may be that is the point of information you should tell the House that kama ni kifua kinakusumbua, *that is what the Honourable Member has asked.*

Hon. Katana: Thank you Mheshimiwa Spika, it is in record of this Honourable House that I am asthmatic and it is known because the Human Resource has all the records so am not mentally ill, I think that will be a good reply to the witch doctor. Thank you.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much and I think what you have said it is even wise to the House. Thank you very much, yes Honourable Hamida Noor please make your contributions.

Hon. Noor: Thank you, Mr. Speaker, for giving me this opportunity, I want to welcome the students from Mtopanga...

[Interruption]
[Hon. Noor inaudible]

The Speaker (Hon. Khatri): Mheshimiwa, *sound please?*

Hon. Noor: Your MCA is a very good friend of mine, and we sit with him in the Finance Committee. Mr. Speaker, mine is to talk about the finance side and being the Vice-Chair for Finance I want to say that this is a very important forum for us because when we go for our public participations, when the executive have done their part it seems like they do not give the full information to the *wananchi* so, we ourselves as the MCAs are the ones who will clarify for them because in the ADP, when we give our ADP for the five years, they are the ones who are

supposed to be implementing this and we are supposed to be doing our legislation in the County Assembly. Mr. Speaker, I do stand to support this Motion with a very open-minded and open heart so that our *wananchi* can get their full information from the executive and when we go for our public participations, when we sit with our *wananchi* who are right now not immoral and they do not want to participate with us, that they have their full information. Thank you so much.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Honourable Hamida Noor. Yes, Honourable Bernard Ogutu from Changamwe Ward.

Hon. Ogutu: Thank you, Mr. Speaker. Mr. Speaker Sir, allow me to join my colleagues in welcoming the students from Mtopanga Secondary School. Mr. Speaker, I want to urge them that in this learning spree at the end of this session they pick something to go home with. Number two, Mr. Speaker, I was wondering why somebody of sound mind could oppose this Motion, Mr. Speaker...

[Applause]

Mr. Speaker, this Motion is not brought in the floor of the House maybe as a witch-hunting spree! Mr. Speaker, this Motion will give us an opportunity to interact, an opportunity for interaction between the Assembly, the Executive and the people we represent, Mr. Speaker. So, anybody with sound mind should not fear that...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Honourable Bernard Ogutu, I think you are not supposed to discuss about other Members, any Member who is in this House, he can rise and give his opinion. So, it is upon you to give your opinion on the Motion and tell us whether you are opposing or supporting the Motion, but it is not in order for you to discuss about the other Member.

Hon. Ogutu: Thank you, Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Khatri): You never know, maybe people from Shanzu are the ones giving him that message. So, you tell us about yourself and your people from Changamwe and what they want to hear or what they want in their respective word. Yes, you may continue.

Hon. Ogutu: Thank you, Mr. Speaker. Mr. Speaker, I'm well guided but again, I'm the Chair of the Committee on Health; that we must look at mental health issues and for your information the mental health issues are on rise. So, I think we should...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Katana.

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika, nimesimama nikitaka kueleza hivi; nafikiri katika ratba yetu ya leo hakuna chochote kinacho husiana na maswala ya afya. Labda Mheshimiwa Spika awe anasema kuna moja ama mbili ya mazungumzo yaliyoongewa yakagusia maswala ya afya hapa alitaja. Mheshimiwa Spika, nataka kukaa kwa kusema hivi; hii kitu kuonekana vile inavyoenda ni kwamba inaweza kupita lakini ukweli wa mambo tunakimbia majukumu yetu na tunataka kuweka lawama nyuma kwa wananchi na ilhali sisi ndio wagonjwa wa afya na nikisema sisi sio mtu mmoja, sisi ndio tufanye kazi zetu mashinani. Ahsante Mheshimiwa.

Hon. Speaker (Hon. Khatri): Thank you. Yes, Honourable Ogutu. You may continue.

[Interruption]

Yes, Honourable Priscilla Mumba. Are you on a point of...

[Interruption]

About what?

The Chief Whip (Hon. Mumba): Mheshimiwa Spika sisi ni wagonjwa wa afya. Mheshimiwa Spika, hebu atoe msamaha katika neno hilo kwa sababu hakuna mgonjwa ambaye yuko hapa, hatukujitangaza wakati tulipokuwa tunazungumza wala kuchangia hii hoja, ikiwa yeye ni mgonjwa wa akili ni yeye lakini sisi sio wagonjwa wa afya, hatukuzungumza hayo.

The Speaker (Hon. Khatri): Nafikiri Mheshimiwa, hapo ungeweza kujizungumzia wewe mwenyewe kama ni mgonjwa ama si mgonjwa. Mimi naweza kuwa ni mgonjwa wa afya hapa huwezi jua, hivyo basi wakati ukizungumza Mheshimiwa labda useme wewe si mgonjwa wa afya, huwezi kujua wengine kama ni wagonjwa ama si wagonjwa, nafikiri nitampatia Mheshimiwa Ogutu kutoka Changamwe atoe maoni yake. Naam, Mheshimiwa Ogutu, unaweza kuendelea.

Hon. Ogutu: Thank you, Mr. Speaker. Mr. Speaker, I want to bring to the attention of the House that this week is a mental health week so anything that you discuss surrounding that is very important. Mr. Speaker, back to the Motion; in the first Assembly there used to be Town Hall meetings which I think is equivalent to what Honourable Madialo is suggesting, there were times when people could discuss issues and came up with solutions at the meeting. So, when the issues were brought to the House they were already solved at the ground so the forums are very much important. So, I think we should not even spend much time and if you look at the mood of the House this is a Motion that should be passed immediately and the implementation part of it should also be taken seriously, Mr. Speaker. Thank you.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Ogutu. Honourable Members, I just want to give you a point of information; that Honourable Member, *wakati tunazungumzia Mswada*, let us not make it personal *kwa sababu kila mmoja anajua vile amekuja katika hili Bunge na kila mmoja yuko na maoni yake na yule ambaye amelea huu Mswada ambaye ni Mheshimiwa Madialo ama Mswada wengine wowote. Ikifika mwisho yeye anapatiwa wakati kujibu ama kujieleza kwa yale maoni ya watu ambayo wameyaleta ili awezekutia imani watu waweze kumsaidia kupitisha ama sio hivyo kawaida inakuwa Mswada unaanguka. Ningeomba tuangalie yale ambayo yameletwa hapa na kila mmoja yuko na maoni yake na itakuwa sio vyema leo kama tutafanya issue iwe personal*, utapata labda mtu mwengine yuko na maoni mazuri pia lakini anaogopa kuwa akiongea kwa hivyo ningeomba tu tujaribu kila mmoja alete maoni yake alafu tuone vile tutaendelea. Yes, Mheshimiwa Kai Junda *Ward*? Mheshimiwa kwanza utueleze hiyo ni nini umevaa?

Hon. Kai: Ni Kanzu? Ni viazi la dini.

The Speaker (Hon. Khatri): Serjeant umeweza kuangalia kama hiyo ni kanzu Mheshimiwa amevaa?

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Oh, ni kanzu ya Kiislamu, sawa.

Hon. Kai: Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwanza nianze kwa kuwashukuru na kuwakaribisha wasomi wa shule ya upili ya Mtopanga ambapo kwa wingi wengi wanatokea maeneo ya Junda. Hivyo ni wapitishie salamu ya kwamba Mheshimiwa Morgan mara nyingi sana akiwa hapa anazungumza maneno ya maendeleo ya kuhusiana na elimu lakini pia pamoja na miundo misingi. Mheshimiwa Spika, nataka nizungumze kidogo kuhusu vazi langu hili kwa nini mara nyingi hukunjana hili vazi; kwanza hili ni vazi ambalo linaruhusiwa kwa sababu ni vazi la dini na hapa tunaruhusiwa kukunja na mavazi ya dini lakini pia mavazi ya kitamaduni. Mimi katika Wadi yangu ninatangamana sana kwa wingi na ndugu zangu wa Kiislamu na hawana mwakilishi mwingine isipokuwa wale Waislamu ambao nawakilisha vile vile bado mwakilishi wao wa Junda ni mimi.

Kwa hivyo hii inavaliwa kuonyesha uwiano na utangamano kati ya Waislamu na wakristo walio kondani ya Junda. Nikiweza kurudi katika mada hii tuliyo nayo Mheshimiwa Spika nataka niweke wazo kurudi kwa ni hoja nzuri na naiunga mkono asilimia mia moja. Kifungu cha kwanza cha katiba ya Kenya kinasema kwamba nguvu kuu ziko na mwananchi. Na tukiangalia kwa sasa hivi Mheshimiwa Spika vijana wa kizazi cha za almarufu ‘Gen Z’ kwa sasa hivi wamekua kwa ukubwa wakilalamikia ya kwamba serikali yetu ya leo imekosa kuwahusisha kikamilifu katika maswala yanayohusu jamii lakini taifa kwa ujumla na ndio sababu licha ya kwamba sisi kama wajumbe tumepewa fursa ya kuwakilisha matakwa ya wananchi sisi, hata wakati wowote ule, tunapoweza kupitisha Miswada, huwa inafikia mahali ambapo tunahusisha jamii, tunapoita *public participation*.

Hivyo basi sisi kuongeza nafasi hususan ya kuona kwamba wananchi wanahusishwa zaidi, haiwezekani kwamba ina makosa yoyote, bali ni kuhakikisha ya kwamba wananchi wanapata fursa ya kuelewa wajumbe katika Jumba hili wanazungumzia maswala gani ikizingatiwa Mheshimiwa Spika kwamba huwa hatuna ile *live coverage*, kwamba wananchi wetu, wataweza kufwatilia yale mambo ya msingi tunayoweza kuyazungumza hapa. Kwa hivyo nisiwe mrefu wa maneno, bali niungane na wale Waheshimiwa wote wengi wa hekma ambao wameweza kuunga mkono mswada huu. Shukran sana Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Kai. Yes, Honourable Maimuna Salim please make a contribution.

Hon. Maimuna Salim: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia kufika hapa; pia nawashukuru watoto kutoka Mtopanga ambao wamekuja kuona zile shughuli ambazo tunazoendesha na walimu. Nimesimama kuunga mkono hoja hii. Mheshimiwa Spika, kuna malalamishi mengi sana ya kwamba sisi vile tukipitisha bajeti, tunajua ya kwamba kuna miradi ambayo inaendelea mashinani, tukienda kufanya oversight, hiyo miradi hakuna. Lakini tukishirikiana na wananchi kulingana na hoja hii ilioretwa na Mheshimiwa wa Mikindani itakuwa pia sisi kazi zetu zitakuwa ni rahisi. Kwa sababu mwananchi kile alichokiomba itakuwa ndio anastahili kukipata na kabla hatujaenda kwa *next financial budget*, itakuwa tunaangalia *last financial budget* tulipitisha kama barabara tano na ECDE katika Wadi ya Mtopanga je, hizi barabara tano ni gani, na zilifanyika wapi, na shule ile ambayo tumejenga ya ECDE, ilikuwa inagharimu pesa ngapi, na imeisha?

Ndio tuweze kuangalia miradi gani mengine. Kwa hiyo, mimi nimesimama kuiunga mkono Mheshimiwa Spika kwa sababu itatufanya sisi kama Waheshimiwa tuweze kuonekana na wale wananchi wetu ya kwamba tunawajali na tunawaenzi sana lakini kuna mahali kwengine huwa tumekakwa mabawa. Lakini tukiweza kwenda hivi tukishirikiana na wananchi wetu, tutakua tunafanya *oversight* yetu vizuri na ikija kwa upande wa *legislation*, kwa Bunge pia tunafanya vitu ambavyo tuna uhakika navyo.

Kwa hivyo, Mheshimiwa Spika mimi nimesimama kuiunga mkono na nina imani ya kwamba tukienda hivi, basi watu wa Mombasa wataweza kuwaregesha wale ambao wamechaguliwa, kulingana na utenda kazi wao na itakua kuna *transparency* katika miradi. Kwa hivyo, nimesimama kuiunga mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes, Honourable Leila Nyache from Kipevu Ward please make your contribution?

Hon. Nyache: Ahsante sana Mheshimiwa Spika nami kuweza kuniona ili niweze kuchangia Mswada huu. Kwanza nachukua fursa hii kuwakaribisha watoto wa kutoka shule ya upili ya Mtopanga, secondary school, nawambia kwamba karibuni sana, muone yale waheshimiwa, wanafanya, ama wanawakilisha, wananchi wao, huko mashinani nataka niwambie, Mheshimiwa Morgan anasimama na Mtopanga kama kazi, na hachekei na kazi, anaangalia watu wake vizuri sana. Nikija kwa hoja hii iliokuja na Mheshimiwa Madialo nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Madialo kwa hii hoja, aliokuja nayo. Kwa kweli hoja hii Mheshimiwa Spika ni kama hamasisho la kuweza kuhamasisha wananchi mashinani waweze kujua, kazi ya *executive* ni gani na kazi ya MCA ni gani na hiyo Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana kwa sababu hii hoja kwanza itaweza kutuina sisi kama MCA's naitaweza kutufunua uso. Kwa sababu, lawama zimezidi mashinani miradi ambayo haijaisha, tunaambiwa ni sisi miradi imefanyika haijaisha, tunambiwa ni sisi. Kwa hivyo...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Katana, were you on a point of information?

Hon. Katana: I'm not sure whether it will be a point of order or a concern, because I'm not seeing anywhere that this meeting, the meeting that we are advocating for will be a meeting to let the public know our duties, the duties of the of the executive as she has said.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you. Yes, Honourable Leila.

Hon. Nyache: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mimi naona Mheshimiwa mwenza, sijui kama amenielewa vipi kwa sababu mimi nimesema hii hoja inaweza kujulisha wananchi mashinani ya kwamba kazi yetu ni ipina ya *executive* ni ipi. Kwa sababu, ile miradi inayoletwa kule mashinani na haishi wananchi kuelewa. Najua ni sisi MCA, sasa tukifanya kwa kweli ya hii mikutano hii ya kuita wananchi na tuweke uwazi, wataweza kujua kweli hiyo sio kazi yetu ni kazi ya *executive* na hii itashiria hawa *executive* waweze kuwajibika katika kazi yao, na kwa kweli, itaweza kuleta natija katika Mombasa yetu nampongeza sana, Mheshimiwa Madialo na mimi namwambia tu ameleta hoja mzuri sana ya kuweza kutuina sisi MCA na pia kututolea ile dharaui sisi tunadharauliwa na wananchi mashinani na zile lawama pia zitatuondokea kupitia hoja hii. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Leila. Yes, Honourable Pamela Ojala, please make your contributions.

Hon. Ojala: Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity also to give my contribution. Allow me before I proceed with my contribution Mr. Speaker, I want to express my deep appreciation to you as our Honourable Speaker, you made us proud as women of this County for being with us as a dad, as a friend and a boss and we cannot take it for granted Honourable Speaker, may God bless you abundantly.

Honourable Speaker, when I am back on the discussion, I want also to join my Honourable colleagues for welcoming students from Mtopanga. Mr. Speaker, I stand to support the Motion on annual Sub-County multisectoral public engagement forum, Mr. Speaker. Mr. Speaker, this is a very important Motion before us this morning, and I want to congratulate my colleague from Mikindani, Honourable Madialo for bringing this good Motion to this Honourable House. May we give him a big applause, Mr. Speaker because he deserves it. Again, when you check this Motion Mr. Speaker, it will give active participation, it will also provide valuable content and it will also foster a sense of commitment because I do not want to dwell more on this Motion because it is well elaborated. I stand to support the Motion Mr. Speaker, thank you very much.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you. Yes, Honourable Maryam Baimu from Frere Town Ward, please make your contributions.

Hon. Baimu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza ningependa kuwakaribisha wanafunzi wetu kutoka Mtopanga. Karibuni sana katika Bunge hili na pia ningependa kumpongeza MCA wenu Mheshimiwa Morgan kwa kazi nzuri ambayo anafanya, karibuni sana wanafunzi. Pili, ningependa kumpongeza Mheshimiwa Madialo kwa hoja hii; nimesimama kuunga mkono kwa sababu tunajua sote kule mashinani kuna shida kubwa wananchi ile imani yao kwetu sisi kama viongozi imeshuka sana sababu wanasema kwamba walituchagua sisi kuja kuwakilisha hapa lakini tuna ahidi vitu vingi na zikapita kwa hio ADP ya mwaka jana lakini wanaona hakuna kitu kimefanyika na kama kimefanyika pengine hakijamalizika. Kwa hivyo ni muhimu hivi vikao kama vitafanyika ili wananchi waweze kuelewa majukumu ya MCAs ni gani na ya utawala ni gani na wao kama wananchi hoja zao wanavyozipitisha pale katika hio ADP waweze kuzifuatilia ama waweze kuulizia utawala pengine mahali gani wamefikia. Kusema kweli tuko na jukumu kubwa, wakati wetu kama MCAs unaenda ukiisha kwa awamu hii; kwa hivyo ni muhimu Mheshimiwa Spika watu tuweze kusimama imara, mda uliobakia tungangane ili angalau hadhi yetu kwa wananchi kule iweze kurudi, wajue walichangua viongozi ambao waliwajibika mwaka unaofuata 2027 palipo uzima na uhai, wawe na imani na sisi na Mungu akipenda tuweze kurudi katika hili Bunge ili kuwakilisha watu wetu Mashinani. Ahsante sana Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Madialo, naunga mkono hoja hii.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you. Thank you very much Honourable Baimu. Yes, Honourable Mwaka Mulundonda.

Hon. Mwaka Mulundonda: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Kwanza nataka kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae ametupatia wikendi njema na tumerudi katika hili Jumba. Pili, nataka kuwakaribisha wanafunzi wa kutoka Mtopanga pamoja na Mheshimiwa wenu ambaye amesababisha mkafika hapa mje muone Jumba hili linavyoendelea na kuwa viongozi wanafanya nini. Mmepata Mheshimiwa mzuri Mheshimiwa mwenye umri wake takriban mzuri yeye mwenyewe ni mzuri, saa yote anacheka sijui kama anakasirika wakati mwengine anatabasamu kila saa. Tabasamu yake naona mnaiona wanafunzi. Pili, nataka kumshukuru Mheshimiwa wa Junda hapa na wa Mikindani najua vile Mheshimiwa Spika amesema umevaa kanzu ama ni dera sasa nalitazama vizuri lakini kumbe ni kanzu. Nashukuru sana kuleta hoja hii ni hoja ambayo ni ya maana sana yenye kutujengea na ni hoja ambayo kwamba inatuvua angalau na sisi kutuweza kupata majukumu kuwapatia wananchi ili wajue sisi Waheshimiwa tuna kazi zetu maalum na kazi zengine ambazo kwamba zinawasaidizi kama Sub County Administrator, ward administrator na pia vile vile *village administrator*.

Kwa sababu tutakuta kazi nyingi ambao kwamba zinafanywa tunazichukua majukumu ya wote tunajibebesha sisi wenyewe lakini leo hii kulinganana hii hoja ninaona itaweza kutusaidia sana ikiwezekana tuiptishe kwa pamoja na tuweze kufwatilia ili iweze kufanya kazi. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes, Honourable Hawa?

Hon. Hawa Omar: Thank you, Mr. Speaker, for giving me this opportunity to contribute to the motion. Allow me to welcome the students from Mtopanga Secondary represented by Honourable Morgan Matsaki. Feel welcome. Feel free to ask any question for you are the future generation. Secondly, I would like to congratulate Honourable Jactone Madialo from Mikindani ward for coming up with this Motion, very important Motion and also like to be on record that I support for the purpose of transparency and accountability. Thank you, Mr. Speaker I stand to support.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes, Honourable Patrick Mbelle from Bamburi Ward. Please make your contributions.

Hon. Mbelle: Shukran Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika kwanza ningetaka kusema kwamba naunga mkono hoja hii ingawaje ningependa pia kusema kwamba kuna upande fulani na muunga mkono Mheshimiwa Katana aliposema kwamba majukumu mengine ni yetu sisi kama Waheshimiwa waliochaguliwa ili kuweza kutekeleza...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Mheshimiwa Patrick Mbelle ni aidha unaunga mkono ama unapinga kwa sababu hapa hoja ni moja na imeletwa na Mheshimiwa Madialo na Mheshimiwa Katana aliweza kutoa maoni yake kwa hivyo ni wewe useme unaunga mkono ama huungi mkono lakini huwezi kuja kwenye floor of the house useme naunga huku na huku so ni utuambie waunga mkono ama unaweza kumuelekeza mwenye aliyoleta hoja afanye marekebisho kwenye motion yake ili hali iweze kuleta yale maoni yako ndani so Mheshimiwa Patrick Mbelle endelea.

Hon. Mbelle: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa yale ambayo umeniambia ingali Mheshimiwa Spika nilikuwa najenga hoja na ilikuwa sijafikia mahali pa kusema kwa nini nimeunga upande huu na kwa nini pia maneno kathi ya hal ambao yalisemwa nimeza kuyapokea na kueza kuunga mkono. Mheshimiwa Spika hoja iliyoletwa leo hii inatowa mwongozo mpya katika utendakazi wa serikali nzima kwa jumla. Ambapo ni sisi Waheshimiwa, *Executive* na vile vile hata wananchi wa kuwa mbao ni baadhi ama wahusika wakuu katika serikali. Mheshimiwa Spika hoja hii imesema kwamba anataka tu wawe na vikao katika kiwango cha Sub County. Sisi tuliochaguliwa hapa ndani Mheshimiwa Spika kazi yetu ni kuangalia maswala katika Wadi kwa hivyo vikao hivi vinapokuwa katika kiwango cha Sub County inatupea nafasi ya kuweza kujua katika Sub County zetu ambapo tunaketi Waheshimiwa sita, saba nane ni yapi ambayo yanatudhuru sisi sote tukiwa kwa pamoja na tunaweza kushughulikia kwa pamoja ili tuweze kuyatimiliza kama vile wananchi wanasema. Mfano Mheshimiwa Spika ni kwamba iwapo leo hii nina shida ya maji katika Wadi yangu ya Bamburi maji katika Wadi ya Bamburi hayatoki katika sehemu ya Bamburi Ila matanki haya katika sehemu ya Mwakirunge. Kwa hivyo kuna umuhimu wa mimi kushirikiana na Mheshimiwa wa Mwakirunge ili kuhakikisha kwamba maji yanaweza kunifikia kwangu ndio nasema kwa *cross border projects* lazima ziwe na sehemu ya watu kukaa chini na kuongea. Vile vile Mheshimiwa Spika nichangie kwa kusema kwamba hoja hii ni muhimu kwa sababu sisi kama Waheshimiwa hatuna muda wa kusema kwamba tuna uwezo wa Mwenyezi Mungu wa kuwa kila mahali kwa wakati wote.

Kwa hivyo ni muhimu saa zingine kuweza kukaa chini kwa pamoja na wananchi kuweza kusikia yale ambayo hatujasikia ama kuyaona katika macho yetu ama nguvu zetu za kibinadamu kuweza kuyapata yote kwa pamoja. Vile vile Mheshimiwa Spika tunapotengeza bajeti, bajeti ile ni sheria na sheria ile inafaa ifuatwe kulingana vile ilivyowekwa Mheshimiwa Spika kuna wakati ambapo Serikali ya Kaunti inashinda kufuata sheria hii labda saa zengine kwa ukosefu wa fedha ama kwa fedha kuja kwa kiasi cha kidogo kulingana na vile ilikuwa tumepanga lakini Mheshimiwa Spika haimaanishi hiyo ni sababu ya Serikali ya Kaunti kushindwa kutekeleza miradi, inafaa iwe inapata nafasi kuweza kuwa na kuelezea wananchi ya kwamba tulipangia kutumia shillingi kumi lakini tumepata shillingi saba, na ndio maana tumeshindwa kutekeleza majukumu moja, mbili ama tatu, ndio mwananchi naye awe na uweza wa kuweza kuomba miradi hio katika miaka ambayo inakuja katika maswala ya bajeti.

Vile vile Mheshimiwa Spika ripoti zinapotoka katika mijadala ile ama mikutano ile, itatusaidia sisi kama Waheshimiwa katika Bunge hili, kuweza kutumia ripoti hizo kutengeneza vitu vya maana kama vile bajeti ama hata kufanya usarangi ama *oversight* katika serikali ya Kaunti, ili kujua ya kwamba yale ambao wananchi wanataka wanaweza wakapata. Mheshimiwa Spika vile vile nikimalizia ni kwamba, tunapo tengeneza bajeti Mheshimiwa Spika, mara nyingi tunatengeza bajeti kwa yale ambao tunayajua sisi kama Waheshimiwa na yale ambayo *Executive* wanataka, lakini kwa hali ya angaa na hali ya mustakabali katika jamii zetu hubadilika kila siku na ndiposa ni muhimu kwamba tuwe na nafasi ya kuweza kuketi chini na wananchi kuweza kuwasikiza wanayotaka wao, kuweza kusikiza ni wapi tumewaudhi ama tumewakosea na kuweza kuwasikiza vile vile ni yapi wangetaka tuweze kuwasuluwisha sisi kama Waheshimiwa wakati bajeti inapoendelea kutekelezwa. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika niseme ahsante, ninaunga mkono hoja hii na nikisema kwamba yale aliyosema Mheshimiwa Katana hajakosea iwapo, Mheshimiwa Madialo amesema kwamba tuwe na vikao katika level ya Sub – County si katika level ya Wadi na ndiposa, tuweze kuwa na maneno haya kuweza kuongea kwa jumla kama Waheshimiwa. Ahsante Mheshimiwa Spika.

[Applause]

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Patrick Mbelle. Yes, Honourable Jactone Madialo the Motion mover? You may now reply to the Motion thank you.

Hon. Madialo: Ahsante Mheshimiwa Spika na pia ningependa kuchukua fursa hii kushukuru Waheshimiwa wote pamoja pia na Mheshimiwa Katana, kwa sababu ya kuchangia hoja hii kwa dhati na pia Waheshimiwa wengi karibia wote wamekubaliana na hoja hii. Ningependa kusema hivi kwa haraka Mheshimiwa Katana amesema kwamba sisi kupitisha hoja hii ili tuwe na vikao ni kana kwamba tunawaambia wananchi kwamba tumeshindwa na kazi yetu! Nashukuru maana Mheshimiwa Mbelle amegusia kile ambacho ningependa kugusia kwamba nataka kumwambia Mheshimiwa Katana hukuchaguliwa kwa sababu wewe ndio bora kuliko wote Shanzu, hukuchaguliwa kwa sababu wewe ndio mwerevu kuliko watu wote Shanzu, hukuchaguliwa kwa sababu wewe ndio unajua Shanzu yote, vichocho vyote kuliko watu wote bali ni neema ya Mwenyezi Mungu ndio ilikuleta hapa. Kwa hivyo tunapoenda kwa wananchi ni kwa sababu kuna wananchi na kuna mambo mengine wanaweza jua ambapo sisi hatuwezi jua. Nataka kukupatia mfano mmoja; siku ya jumapili jioni jumamosi jioni nilipigiwa simu nikaambiwa kwamba, pole nikamuuliza kwa nini huyu mtu ananiambia pole kwa sababu gani, alijaribu kunipigia lakini nilikuwa mteja akani *text* kwa *Whatsapp* akaniambia pole. Nikamuuliza pole kwa sababu gani, akaniambia si watu wanne wamekufa katika Wadi yako...

[Interruption]

Ngoja kidogo, naomba Mheshimiwa Spika unilinde...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, you can continue?

Hon. Madialo: Ahsante, kwa hivyo alivyonieleeza ndio akaniambia kwamba kuna mkurupuko wa *cholera* Kibarani. Kwa hivyo saa zengine kwa nini maana mtu ambapo yuko huko sasa ndio amenijulisha, maana vile huyu amesema wewe sio Mungu ama mimi si Mungu ambao tunaweza kuwa kila mahali kwa wakati mmoja. Kwa hivyo hii itatusaidia kwa wananchi ambao; kwa mfano huyu Mheshimiwa wa Junda Wadi yake ni kubwa sana kimaeneo pamoja na Mwakirunge na hata Mheshimiwa Joshua wa Jomvu huwa anapenda kusema hivi ya kwamba Jomvu Kuu ni kubwa kuliko eneo Bunge la Changamwe, Wadi ya Mheshimiwa Joshua. Kwa hivyo huwezi...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Honourable Jactone Madialo, please when you are on the floor of the House address the Speaker, I can see now you are addressing the Honourable Members *ama labda nije nikupishe hii Kiti hapa ukalie.*

Hon. Madialo: Well guided Sir. *Kwa hivyo Mheshimiwa Spika hii ndio sababu, nimeongea kama dadangu na pia Mheshimiwa Katana amesema hata zile Public Participation za ADP na budget watu huwa hawaji na namuunga mkono kwa sababu, ile vile watu hawaji ni kwa sababu ni baada ya serikali kwenda kwao kuwapatia ADP na Budget hawatarudi tena kuwaelezea jinsi vile wamewafanyia maendeleo watarudi tu tena wakati ule wa ADP na Budget baada ya Mwaka mmoja ndio maana hii forum itapeanwa nafasi kwa wananchi kuuliza moja kwa moja. Mheshimiwa Kiongozi wa Wengi amesema kwamba italetwa katika Sub-County na Sub-County officers na Ward Admins ndio wawe hapo kuwaelezea. Tunataka hii by the passage of this Motion, tunataka wale Ward Admins na Sub-County Admins na Waheshimiwa MCA's kazi yao iwe ya mobilization lakini si hao Ward ama Sub-County Admins waje hapa kuelezea watu. Tunataka department zote katika hio mikutano...*

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Katana? Are you on a point of information?

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika nimeiangalia hii hoja yetu ya leo katika maombi yote manne yaliyoletwa hakuna ombi ambalo limesema sisi tuwe *mobilizers* za watu wanaokuja katika hii mikutano. Alafu Mheshimiwa Spika ikiwa wewe mwenyewe simu unaweka *flight mode* kwa sababu uko na *Wifi* na unaweka *Whatsapp* pekee yake, watu watajuaje ama watakupataje ndio ujue kwako kume poromoka Mheshimiwa Spika ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Madialo you may continue.

Hon. Madialo: Honourable Speaker, I can now confirm that the Honourable Member is unwell, I can now confirm.

[Laughter]

[Applause]

Hon. Madialo: Na mimi ninaomba Mheshimiwa Spika Bunge litakapo...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): But Honourable Madialo I think the Honourable Member himself, confirms that he is unwell...

[Interruption]

Hon. Madialo: Ile *confirmation* yangu sia ya pumu, *confirmation* yangu ni ya akili.

The Speaker (Hon. Khatri): No, I think Honourable Madialo you are out of order! Yes, Honourable Katana?

Hon. Katana: If I can be sure Honourable Speaker, if I can cite a Standing Order number I guess it is (87) which says '*Whenever a Honourable Member stands to say something must substantiate*' Honourable Speaker, I have gone a number of times for tests because of some things that maybe unknown to you Mr. Speaker, now the Honourable Member from Mikindani substantiate wherever the allegation he has made about me. Thank you.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Jacktone Madialo you may either substantiates wetever you have said or withdraw and apologise.

Hon. Madialo: Honourable Speaker, as a man who fears God I apologise and withdraw.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Hon. Member.

[Applause]

Hon. Madialo: Sasa ilikuwa hoja yangu ilikuwa naendeleza kwa kingereza kwa hivyo nishamjibu ama nishatoa wasi wasi kwa Mheshimiwa Katana, Kiswahili? Sawa Kiongozi wa Wengi alivyosema kwamba ni wale Sub-County na Ward Administration hao tu watumike kuleta watu pamoja na Waheshimiwa. Mheshimiwa Katana amesema kwamba hakuna kwa hoja hii mahali inaonyesha ya kwamba ni Waheshimiwa wakapate kuleta watu, si mambo yote lazima yaandikwe moja kwa moja, kwa sababu kama kuna kikao lazima hao watu watakuja ama wataletwa ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Mbelle ameongea kuhusu Sub-County ile sababu nikaonelea wacha ifanywe kwa Sub-County kwa sababu ikifanywa kwa *Ward* kwa mfano, inaweza kuchukua zaidi ya Mwaka mmoja maana Wadi ziko thelathini, lakini ikifanywa kwa Sub-County pengine maana mwaka uko na miezi kumi na mbili na Sub-County ni sita, labda mara moja baada ya miezi miwili inaweza kuwa inasaidia. Alafu mwisho pia ningependa kumshukuru...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Katana?

[Interruption]

Please one-minute Honourable Frankline let the Honourable Member. Honourable Frankline Makanga has a seat please.

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika kwanza kile kifungu anataka kusimama nacho ni kile cha kusema nisisimame mara kwa mara lakini nataka kuongea kitu cha maana na kama utaongea kitu kingine ninyamaze saa hii. Mheshimiwa Madialo, mimi nataka niseme hivi Mheshimiwa Spika hapa ombi la kwanza na la pili, limesema mambo na *annually* ikasema mambo na *once per year*.

Saa hii tunabadilika tena after miezi mbili Mheshimiwa Spika chini ya hekima ikiwa tunapelekwa kama makondo itakuwa si sawa na hili Jumba ni la mpangilio. Mheshimiwa Spika, ukisoma ombi lake la tatu na nitalisoma kwa kingereza kwa maana limeandikwa. Mheshimiwa Spika naomba huyu mtu mfupi akae ili niendelee.

The Speaker (Hon. Khatri): Honourable Katana, please you have to withdraw that, there is no one in this House who is called *mtu mfupi hapa*.

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika, naomba msamaha ili nipate nafasi ya kuweka hoja yangu ya maana.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes.

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika, ombi lake la tatu.

Hon. Makanga: I request Honourable Allen Katana to sit down.

The Speaker (Hon. Khatri): It is okay Honourable Frankline. I will give you a chance, it is okay you will put it in the right place when he finishes to give his contribution yes Honourable Katana?

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika ombi la tatu inasema, *'The County Secretary develops an issues clear guideline on how the forum will be conducted, beginning with 2025/2026 financial year'* sasa mimi kwa mtazamo wangu labda hii hoja Mheshimiwa wa Mikindani, amefanya kuandikiwa kutoka Homa Bay akaja akaileta hapa bila hata yeye mwenyewe kuisoma, anatupa kazi sisi na kukusanya watu kuwaleta kwa mikutano ambao si jukumu letu. Na kitu chengine Mheshimiwa Spika elewa na nikimaliza, validation sisi wenyewe tunafanya validation under Sub-County Level hatufanyi kwa kiwango cha Ward ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Katana for your point of information. Honourable Makanga, please.

Hon. Makanga: Mr. Speaker, I think it is important that Honourable Speaker you give a direction, he can not walk out of the chamber after making such gross confessions.

The Speaker (Hon. Khatri): But maybe he is going to use the toilet Honourable Member, I cannot stop an Honourable Member.

Hon. Makanga: No Mr. Speaker that is purely an abuse of the powers and privileges in this House. Honourable Speaker, we have very clear Standing-Orders and that is why this House is a House of Laws and Order and by extension a House of records. Honourable Speaker, the conduct by Honourable Allen Katana is violating our own Standing Orders from Standing Order (102) Honourable Speaker his misconduct of pure reputation not to meant add clarity, not to meant to add valid to the debate but Honourable Speaker to create confusion, mislead the House and create a tedious process...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Abdirahman...

Hon. Makanga: Is he an accomplice?

The Speaker (Hon. Khatri): Are you on a point of information?

Hon. Abdirahman Abdikadir: I am on a point of order, I think.

Hon. Makanga: Which Standing order, Honourable?

Hon. Abdirahman Abdikadir: Yes, I think Honourable Frankline, you can just take your seat.

Hon. Makanga: Oh, you are not the Speaker boss and I am on the floor.

The Speaker (Hon. Khatri): Honourable Makanga let the Honourable Member talk.

Hon. Abdirahman Abdikadir: Yes, Mr Speaker I think Honourable Makanga is out of order to discuss the conduct of a Member because before we discuss the conduct of a Member we need a substantive motion, be guided and it also wrong to discuss the conduct of a Member while he is not around. So, Mr Speaker I hope he is guided thank you.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Abdirahman. Yes, Honourable Makanga?

Hon. Makanga: You see Honourable Speaker that is why I said Honourable Abdirahman is an accomplice, because he was the one who was guiding him that now, please walk out of the chambers and you see we can't tolerate such characters.

The Speaker (Hon. Khatri): So, Honourable Makanga, just give your point of information to the House

Hon. Makanga: Yes, now the point of information Honourable Speaker was seeking your directions as the Speaker of this House and as the one chairing this sitting. Honourable Speaker, that we be careful that the Standing Orders here are not violated under your watch, because it must be on record when we have such characters, who only have repetitive...

The Speaker (Hon. Khatri): What Standing Order are you quoting?

Hon. Makanga: (102) Honourable Speaker.

The Speaker (Hon. Khatri): Okay, what is it saying?

Hon. Makanga: It is talking about irrelevance or reputation going down towards (103) on gross disorderly conduct Honourable Speaker, which states situations or times when such things when they happen, then you are allowed to take action Honourable Speaker and this Honourable Speaker, has been manifested here when a Member is replying to his own Motion, a Member again is standing on a point of order which he is not even able to sign the respective orders. Please Honourable Speaker, the accomplice and the accomplice are now rejoining so Honourable Speaker give us directions as we conclude this conversation. Thank you.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Members. Yes, Honourable Patrick are you on a point of information again? Because I want to give the Honourable Madialo to finish but please.

Hon. Mbelle: Mr. Speaker Sir, I wish to inform the House that, Honourable Katana had misled the House by saying that the first point and the second point are of a similar in nature. The first one which is A talks about the establishment of the forum and the second one talks about the mode of conducting that forum, so the establishment of our...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): But Honourable Members just remember the Honourable Member Madialo who is a mover of this Motion, is going to reply and I'm sure he is intelligent enough to tackle whatever the Honourable Members point of information he was given.

Hon. Mbelle: Thank you, Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Khatri): So, let us give time to the mover of the Motion to reply to those points of information.

Hon. Mbelle: Thank you Mr. Speaker. I'm well guided.

The Speaker (Hon. Khatri): Please yes Honourable Ogutu. I thought you were on a point of information as well?

Hon. Ogutu: Yes Mr. Speaker Mr. Speaker, I think we are guided by Standing Orders and there is a precedence we are setting, that may not be well. Mr. Speaker when a Member is responding or replying to a Motion, I believe that nobody should disturb him because they got the opportunity to discuss the Motion while it was on the floor. So Mr. Speaker I think we are setting a precedence that may not auger well maybe in future. Thank you, Mr. Speaker.

[Applause]

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Members for your guidance but, I think Honourable Madialo is smart enough and intelligent to tackle whatever the Honourable Member was saying. So, I will give back to Honourable Madialo to reply to your Motion and please, you may continue.

Hon. Madialo: Thank you Mr. Speaker Sir, I would want to shorten because I'm seeing some tactics that are kangaroo in nature. I would want to school Honourable Katana that once in a year is the totality of it that these forums, it does not matter how many of them and we have proposed that once per sub-County all the six be done in a span of one year. So, it does not mean that annually means that now it is not done in the Sub-County that all of them are done once that is not it.

The Speaker (Hon. Khatri): Order Honourable Katana, please and please as I said Honourable Madialo addresses the Speaker and continue.

Hon. Madialo: Lastly, Honourable Speaker I agree with Honourable Abdirahman and I promise him that if the Honourable Members are kind enough to vote for this Motion, I will join hands with him to take it to the next level the Senate as a petition, so that it is uniform across this nation thank you.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Madialo and Honourable Members for your contributions to this Motion. Honourable Members, I will now put the question that the Motion by Honourable Jacktone Madialo on Annual Sub-County Multispectral Public Engagement Forums be approved by this Honourable House in the same terms as debated and moved?

[Question put and agreed to]

[Applause]

And the Motion by Honourable Jactone Madialo on Annual Sub-County Multispectral Public Engagement Forums is adopted by this House. Yes, Clerk next order please?

ADJOURNMENT

Honourable Members, this House stands adjourned until Tuesday 17th of June, 2025 at 2:30p.m.

The House rose at 1:05p.m.